بِأَيِّ عَقْلٍ وَدِيْنٍ

جَعْلُ الْأَنِيْنِ (آهْ آهْ) مِنْ أَسْمَاءِ اللهِ الْحُسْنَى؟

JE,

NI KWA AKILI GANI NA DINI GANI

KUJAALIA SAUTI YA KUUGUA (Aah Aah) NI KATIKA MAJINA MAZURI YA ALLAH?

Imekusanywa na:

Abu Halima Arafat Bin Mahmoud

UTANGULIZI

Sifa zote njema anastahiki Allaah Mola Mlezi wa walimwengu wote, na Swala na Salamu Zimshukie Mtume Muhammad ﷺ, Mbora wa Manabii na Mitume, na pia Aali zake na Maswahaba zake wote.

Baada ya hayo:

Hakika mengi katika yale wanayoyafanya watu wapotofu, kama Masufi, Mashia n.k na wanayo andika ndani ya vitabu vyao, ni mambo ya uwongo na uzushi wa wazi, ambao haufichiki kwa kila mwenye akili timamu, achilia mbali mtu aliyeshikamana na mafunzo ya sheria tukufu ya Uislamu na mwongozo wa Mtume wake ﷺ .

Miongoni mwa uwongo waliouzusha watu hawa bila kuona haya ni kujaalia kwamba sauti ya kuugua kwa mgonjwa ni katika majina ya Allaah ‘Azza Wajalla, mpaka wakafikia kwa uzushi huu kutunga hadithi ili kuihami bidaa yao hiyo mbele za watu wajinga wasiofuatilia mambo ya kielimu; wakasimama kwenye mikusanyiko yao huku wakijinadi kuwa na elimu ilihali ni wahyi tu na mpulizo wa shetani anaowapulizia wafuasi wake!

Isipokuwa wao wenyewe wametafautiana, kuna waliojaalia huko kuugua kwa mgonjwa kwa sauti ya (آهْ) na wengine wanaona ni kwa sauti ya (أهْ) na baadhi ya Masufi wanadai kuwa hilo ni jina la Allaah la kifuani.

Ndugu muislamu, fahamu kwamba majina yote ya Allaah ni Tauqiifiyya, maana yake ni kwamba hupatikana kwa ushahidi wa Qur’an na Sunnah, kwa hiyo haifai kwa mtu yeyote kuzua jian na kumbandika nalo Allaah Subhaanah, kwa sababu huko ni kumzulia Allaah lile ambalo hajaliteremsha kwa waja wake! Na wanachuoni wakubwa wameandika vitabu vingi wakitaja majina ya Allaah na hutopata jina hilo la (أهْ) au (آهْ), kadhaalika wamebainisha yale yaliyozuliwa katika hayo majina, yote haya ni kwa ajili ya kuihami Dini ya Allaah isipotoshwe na watu mfano huu.

Kwa sababu hiyo nimeandika Makala hii ili kubainisha ubatili wa riwaya zilizokuja kutaja jina hili, kama walivyobainisha hilo Maulamaa wetu wa Ahlis Sunnah, hali ya kumuomba Allaah taufiq na kupatia.

Abu Halima Arafaat Bin Mahmoud.
Markaz Sheikhil Islaam
Pongwe Tanga.

بسم الله الرحمن الرحيم

Miongoni mwa yale waliyoyazusha kauli yao kwamba kuna hadithi ya Aisha رَضِيَ اللهُ عَنْهَا : kwamba Mtume ﷺ alimtembelea mgonjwa ambaye alikuwa anaugua na kutoa sauti ya kulalamikia maumivu, Maswahaba wakamkataza mtu huyo, Mtume ﷺ akawaambia:

"دَعُوهُ يَئِنُّ فإِنَّ الأَنِينَ اسْمٌ مِنْ أَسْماءِ الله تَعَالَى يَسْتَرِيحُ إِلَيْهِ العَلِيلُ"

“Mwacheni alalamikie maumivu, kwa sababu Aniin (sauti ya kuugulia maumivu) ni mojawapo ya jina la Allaah Ta’alaa, ambalo mgonjwa hupata ponyo kwenye jina hilo”[1].

Hadihi hii ni dhaifu kama alivyosema sheikh Albani رَحِمَهُ اللهُ katika kitabu [Dhai’ful Jaami’ Sswaghir (2985)]. Na hiyo inafanana na hadithi nyingine ambayo hukumu yake ni Munkar (mbaya haifai), inasema:

"يَا حُمَيْرَاءُ أَمَا شَعِرْتَ أَنَّ الأَنِيْنَ اسْمٌ مِنْ أَسْمَاءِ اللهِ عَزَّ وَجَلَّ يَسْتَرِيْحُ بِهِ المَرِيْضُ"

“Ewe Humaira, hivi hujui kwamba (sauti ya) kuugua kwa mgonjwa ni jina miongoni mwa majina ya Allaah ‘Azza Wajalla, hupata ponyo kwa jina hilo mgonjwa?”[2].

Amesema sheikh Abdul Rauf Al-Munawi رَحِمَهُ اللهُ :

"لَكِنْ هَذَا لَمْ يَرِدْ فِي حَدِيثٍ صَحِيحٍ وَلَا حَسَنٍ، وَأَسْمَاؤُهُ تَعَالَى تَوْقِيفِيَّةٌ"

“Lakini (jina) hili halijapatikana katika hadithi yoyote sahihi au hasan, na majina yote ya Allaah ni Tauqifiyyah[3]”[4].

Hata sheikh wa Ki-sufi Al-Ghumaari alipozitaja hadithi hizo na kuzifanyia Takhriij, mwisho akasema:

"فَالْحَدِيْثُ مَوْضُوْعٌ"

“Hadithi hii ni Maudhuu”[5].

1- Angali kitabu: [Kanzul ‘Ummaal] (4226).
2- Silsilat Ddhai’fa (3243).
3- Maana yake: hayajulikani mpaka kwa dalili sahihi, wala halichukuliwi katika hadithi dhaifu.
4- Tazama kitabu: [Faidhwul Qadiir] (Jz. 3, Uk. 533).
5- Tazama kitabu: [Al-Mudaawi Li’lalil Jaami’ Sswaghiir] (Jz. 3, Uk. 36).

Akaendelea akasema:

"فَائِدَة: بَعْضُ الشَّاذِلِيَّةِ بِمِصْرَ يَسْتَدِلُّونَ بِهَذَا الحَدِيثِ عَلَى الذِّكْرِ الَّذِي يَذْكُرُونَ بِهِ، وَيُسَمُّونَهُ اسْمَ الصَّدْرِ وَهُوَ آهْ آهْ، وَالحَدِيثُ كَمَا تَرَى..."

"Faida: baadhi ya wafuasi wa Shaadhiliyyah huko nchini Misri wanaitumia Hadithi hii kama ushahidi wa dhikri ambayo wanaisoma, na wanaliita hilo ni jina la (Allaah) la kifuani, nalo ni Aah Aah, na hali ya hadithi ni kama unavyoiona (ya uwongo)"[6].

****

Asili ya neno hili (آه) katika mweko wa lugha ya kiarabu:

Asili yake ni **أَوْهِ** inayotokana na neno **التَّأَوُّهُ** . Amesema Ibnul Athiir رحمه اللهُ :

(أوْهِ): كَلِمَةٌ يَقُولُهَا الرَّجُلُ عِنْدَ الشِّكَايَةِ وَالتَّوَجُّعِ، وَهِيَ سَاكِنَةُ الْوَاوِ مَكْسُورَةُ الْهَاءِ. وَرُبَّمَا قَلَبُوا الْوَاوَ أَلِفًا فَقَالُوا: **آهِ** مِنْ كَذَا، وَرُبَّمَا شَدَّدُوا الْوَاوَ وَكَسَرُوهَا وسكَّنوا الْهَاءَ فَقَالُوا: **أَوِّهْ**، وَرُبَّمَا حَذَفُوا الْهَاءَ فَقَالُوا **أَوِّ**. وَبَعْضُهُمْ يَفْتَحُ الْوَاوَ مَعَ التَّشْدِيدِ فَيَقُولُ **أَوَّهْ**".

"Auhi (أوْهِ): ni neno ambalo husema mtu wakati wa kulalamikia na kushitakia (maumivu), nalo ni yenye kupata Sukuun herufi yake ya Waawu na Kasra katika herufi ya Haau. Na huenda wakaigeuza Waawu kuwa ni Alif (ya madda), wakasema: Aahi (آهِ) (nashitakia) maumivu ya kitu fulani, na huenda wakaitia Shadda na Kasra herufi ya Waawu, na herufi ya Haau wakaitia Sukuun, wakasema: Awwih (أَوِّهْ), na huenda wakaifuta herufi ya Haau, wakasema: Awwi (أَوِّ). Na baadhi yao huitia Fat-ha herufi ya Waawu pamoja na Shadda, wakasema: Awwah (أَوَّهْ)"[7].

Ndugu yangu muislamu, bila shaka umeona asili ya neno hili katika lugha ya kiarabu, kuwa ni neno analotamka mgonjwa wakati wa kuugulia na kulalamikia maumivu anayopitia, wala si katika Adhkaar wala Nyiradi na wala halina mahusiano yoyote na majina ya Allaah Ta'alaa, bali wala si neno la ibada, ndio maana hupatikana hilo kwa mgonjwa muislamu na asiyekuwa muislamu. Kwa hiyo tumebainikiwa kwamba hadithi hiyo si Sahihi wala Hasan, na pia neno hilo halina mahusiano yoyote na Dini wala ibada, kama tulivyoona katika asili yake.

6- Tazama kibabu: [Al-Mudaawi Li'lalil Jaami' Sswaghiir] (Jz. 3, Uk. 36-37).

7- Tazama kitabu: [An-Nihaaya fii ghariibil hadith] (Jz. 1, Uk. 82).

Jambo la ajabu ni kuona baadhi ya Masheikh wa Kisufi wanasema kwamba hili ndio jina kubwa la Allaah **(الِاسْمُ الأَعْظَمُ)**! kama alivyonukuu hilo Sheikh Muhammad Abdis Salaam As-Shuqeiry رَحِمَهُ اللهُ, katika kichwa cha habari kinachosema:

"فَصْلٌ فِي تَرْكِهِمْ لِلِاسْمِ الْأَعْظَمِ الرَّفِيْعِ، وَتَعَبُّدِهِمْ بِالِاسْمِ الأَحْقَرِ الوَضِيْعِ"

[Huu ni upambanuzi kuhusu kuliacha kwao jina kubwa tukufu (la Allaah), na kuabudu kwao kwa kutumia jina duni baya]. Kisha chini yake akasema:

"وَبَعْضُ المُتَشَذِّلِيْنَ يَقُولُونَ: اسْمُ اللهِ الْأَعْظَمُ هُوَ، **آهْ آهْ**، وَهَذَا ضَلَالٌ كَبِيرٌ وَجَهْلٌ فَظِيْعٌ بِالدِّيْنِ وَاللُّغَةِ... وَعَلَيْهِ فَيَكُوْنُ مَعْنَى اسْمِ اللهِ الْأَعْظَمِ عِنْدَهُمْ: أَتَوَجَّعُ، فَلَا حَوْلَ وَلَا قُوَّةَ إِلَّا بِاللَّهِ الْعَلِيِّ الْعَظِيْمِ"

“Na baadhi ya wafuasi wa (twariqa ya) Shaadhiliyyah wanasema: Jina tukufu zaidi la Allaah ni Aah Aah, na huu ni upotevu mkubwa na ujinga mbaya katika Dini na Lugha ya kiarabu... na juu ya (kauli yao hiyo) itakuwa maana ya jina tukufu zaidi la Allaah kwao wao ni (kusema: Aah): Naumia, Laa haula wala Quwwata illaa bilaahil ‘Aliyyil ‘Adhwiim”[8].

Maana ya Laa Haula.... (Hapana hila katika kuacha maasi, wala nguvu ya kufanya twaa’ ila kwa msaada wa Allaah). Angalia ndugu msomaji, ni kweli ikiwa hiki ndio kiwango chao katika kuelewa Dini basi huo ni ujinga mbaya sana, pia lugha ya kiarabu haiwaungi mkono katika upotevu wao huo.

Na kama hivyo imekuja katika fatwa ya aliyekuwa sheikh wa chuo kikuu cha Azhar Muhamad Abul Fadhli **رَحِمَهُ اللهُ** amesema baada ya utangulizi:

"فَإِنَّكُمْ تَسْأَلُوْنَ عَمَّا يَفْعَلُهُ الآنَ بَعْضُ أَهْلِ الطُّرُقِ مِنْ أَبْنَاءِ هَذَا العَصْرِ، مِن اجْتِمَاعِهِمْ صَبَاحَ مَسَاءَ، يُرَدِّدُوْنَ لَفْظَ (**أَهْ، أَهْ**) يَعْتَقِدُوْنَهُ اسْمًا مِنْ أَسْمَاءِ اللهِ، وَيَقُوْلُوْنَ: إِنَّهُمْ بِذَلِكَ يَذْكُرُوْنَ اللهَ سُبْحَانَهُ وَيُسَمُّوْنَ ذَلَكَ: (اسْمُ الصَّدْرِ)".

“Hakika nyinyi mnaulizia kuhusu kile wanachofanya hivi sasa baadhi ya watu wa twariqa kuwafanyia vijana wa zama hizi, nacho ni kukusanyika kwao asubuhi na jioni, (huku) wakiimba Aah Aah, wakiitakidi kwamba hilo ni mojawapo ya majina ya Allaah, na wanasema: wao kwa (neno) hilo wanamdhukuru Allaah Subhaanah na wanaliita ni jina la kifuani, (kuna baadhi ya majina hutamkwa kwa ulimi lakini hili linatoka kifuani)”.

---

[8]- Tazama kitabu: [As-Sunan wal-Mubtada’at] (Uk. 267).

Jawabu:

"الجَوَابُ: أَنَّ هَذَا اللَّفْظَ المَسْئُوْلَ عَنْهُ (أَهْ) بِفَتْحِ الهَمْزَةِ وَسُكُوْنِ الهَاءِ لَيْسَ مِن الكَلِمَاتِ العَرَبِيَّةِ فِي شَيْءٍ، بَلْ هُوَ لَفْظٌ مُهْمَلٌ لَا مَعْنَى لَهُ مُطْلَقًا، وَإِنْ كَانَ بِالْمَدِّ فَهُوَ إِنَّمَا يَدُلُّ فِي اللُّغَةِ العَرَبِيَّةِ عَلَى مَعْنَى التَّوَجُّعِ، وَلَيْسَ مِنْ أَسْمَاءِ الذَّوَاتِ، فَضْلاً عَنْ أَنْ يَكُوْنَ اسْمًا مِنْ أَسْمَاءِ اللهِ الْحُسْنَى التَّيْ أَمَرَنَا أَنْ نَدْعُوْهُ بِهَا"

“Kwamba neno hili (Ah أَهْ) linalouliziwa, lenye kutiwa fat-ha herufi ya Hamza na Sukuun katika herufi ya Haa, si katika maneno ya kiarabu kabisa, bali hilo ni neno lenye kupuuzwa halina maana yoyote. Na kama litakuwa kwa madda (likavutwa: Aah آهْ) basi katika lugha ya kiarabu linafahamisha kushitakia/kulalamikia (maumivu), wala si katika majina ya vitu (fulani), itakuwaje basi kuwa ni jina miongoni mwa majina mazuri ya Allaah, ambayo ametuamrisha sisi tumuombe kupitia majina hayo...”.

Kisha akaendelea mpaka kwenye kauli yake:

"قَدْ أَجْمَعَ العُلَمَاءُ عَلَى أَنَّ أَسْمَاءَ اللهِ تَعَالَى وَصِفَاتِهِ تَوْقِيْفِيَّةٌ، وَلَا يَجُوْزُ لَنَا إِطْلَاقُ اسْمٍ عَلَيْهِ تَعَالَى أَوْ صِفَةٍ لَمْ يَكُنْ وَرَدَ بِهَا الشَّرْعُ، كَمَا أَنَّهُمْ أَجْمَعُواْ عَلَى أَنَّهُ لَا يَجُوْزُ لَنَا التَّعَبُّدُ بَشَيْءٍ لَمْ يَرِدِ الشَّرْعُ بِجَوَازِ التَّعَبُّدِ بِهِ. وَمَعْلُوْمٌ أَنَّهُ - صَلَّى اللهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ - لَمْ يَخْرُجْ مِنْ هَذِهِ الدَّارِ حَتَّى أَكْمَلَ اللهُ لَنَا عَلَى يَدَيْهِ الدِّيْنَ"

“Maulamaa wamekubaliana kwa kauli moja juu ya kwamba majina ya Allaah Ta’alaa na sifa zake ni tauqifiyyah (hujulikana kwa dalili), wala haijuzu kwetu kumpa jina (Allaah) Ta’alaa, au sifa ambayo sheria haikuitaja, vilevile wamekubaliana kwamba haijuzu kwetu kuabudu kwa (ibada) yoyote ambayo haijaruhusiwa na sheria. Na inajulikana kwamba yeye Mtume ﷺ hakuondoka katika ulimwengu huu mpaka Allaah ametukamilishia sisi Dini kupitia mikono yake”.

Akaendelea tena mpaka akafikia kusema:

"فَثَبَتَ بِذَلِكَ بُطْلَانُ عَمَلِ هَؤُلَاءِ العَوَامِّ الَّذِيْنَ انْتَشَرُواْ فِي الْمُدُنِ وَالْقُرَى يَجْمَعُوْنَ النَّاسَ، وَيَعْقِدُوْنَ الْمَجَالِسَ عَلَى ذَلِكَ وَيَتَّخِذُوْنَ ذَلِكَ وِرْدًا مَوْقُوْتًا زَاعِمِيْنَ أَنَّهُمْ يَتَقَرَّبُوْنَ بِذَلِكَ إِلَى اللهِ، وَفِيْ ذَلِكَ إِضْلَالٌ لِلْعَامَّةِ وَنَشْرٌ لِسُنَّةٍ سَيِّئَةٍ فِيْهِمْ؛ لِأَنَّهُ تَعَبُّدٌ بِمَا لَمْ يَتَعَبَّدْنَا اللهُ بِهِ، وَتَسْمِيَةٌ لِلَّهِ بِغَيْرِ أَسْمَائِهِ، نَعُوْذُ بِاللهِ مِنْ فِعْلِ ذَلِكَ أَوِ الْإِعَانَةِ عَلَيْهِ أَوِ السُّكُوْتِ عَنْهُ".

“Kwa hiyo ikathibiti kwa hayo (yaliyotangulia) ubatili ya amali ya watu hawa wasiojishughulisha na elimu, ambao wameenea katika miji na vijiji, wakiwakusanya watu, na kuweka Mabaraza (mikusanyiko) kwa ajili ya jambo hili na wanaufanya kuwa ni Uradi uliowekewa muda maalumu wakidai kwamba wanajikurubisha nao kwa Allaah,

na katika hayo kuna kuwapoteza watu wa kawaida (wasiojishughulisha na elimu) na kueneza baina yao mwenendo mbaya; kwa sababu ni kuabudu kwa kitu ambacho Allaah hakututaka tumuabudu kupitia hicho, na ni kumuita Allaah kwa lisilokuwa jina lake. Tunajilinda kwa Allaah tusifanye hivyo, wala kutoa msaada juu yake, wala kulinyamazia kimya”.

Akaendelea akasema:

"وَمَهْمَا قَالَ زُعَمَاءُ تِلْكَ الْبِدْعَةِ مِنْ قَوْلِهِمْ: إِنَّهُمْ وَجَدُواْ مَشَايِخَهُمْ كَذَلِكَ. فَلَيْسَ فِيْ ذَلِكَ بُرْهَانٌ لَهُمْ فِي الدُّنْيَا، وَلَا مُخَلِّصٌ لَهُمْ عِنْدَ اللهِ يَوْمَ الْقِيَامَةِ مِنْ عَذَابِهِ، كَيْفَ وَقَدْ قَالَ عُلَمَاءُ الصُّوْفِيَّةِ أَنْفُسُهُمْ: كُلُّ مَا لَمْ يُسْتَنَدْ إِلَى الكِتَابِ وَالسُّنَّةِ فَهُوَ بَاطِلٌ؟ وَقَالُواْ: إِذَا لَمْ يُسْتَنَدْ كَشْفُ الْوَلِيِّ إِلَى الْكِتَابِ وَالسُّنَّةِ فَهُوَ كَشْفٌ شَيْطَانِيٌّ...."

“Na hata viongozi wa bidaa hiyo watasema katika kauli zao kwamba: Wao wamewakuta mashekhe wao katika hali hiyo (wanafanya mambo hayo), hawana katika hilo hoja yoyote hapa duniani, wala mwokozi (wa kuwaokoa wao) na adhabu ya Allaah siku ya kiama. Vipi (usiwe upotevu) hali ya kuwa mashekhe wenyewe wa Kisufi wamesema: Kila kitu kisichoegemezwa kwenye Qur’an na Sunnah ni batili? Na wakasema: Ikiwa Kashfu (ufunuo)[9] wa Walii haikujengwa juu ya Qur’an na Sunnah basi huo ni wahyi wa shetani?...”[10].

Kama hilo halitoshi basi hii Fat-wa nyingine ya kukataza kufaa kumdhukuru Allaah kwa neno hilo la Aah آهْ, aliyoitaja sheikh wenu wa Ki-sufi Al-Ghumaary, (au nayeye hana elimu na ufahamu?!):

9- Kashfu kwa Masufi ni sheikh kufikia daraja la juu la taqwa mpaka huondolewa pazia katika moyo wake moyo wake na macho yake, akawa anaona na kuyajua mambo ya ghaibu (yaliyofichika), na wengine huonyweshwa mpaka yaliyo katika Lauhil mahfuudhi!, kwa hiyo ibada zao nyingi zimejengwa juu ya msingi huu, sheikh wao akiamrisha jambo fulani hata kama liko nje ya mafunzo ya Uislamu watalifanya, kwa sababu amepata Kashfu, hali ya kuwa ni uwongo wa shetani; kwa sababu Dini imekamilika, vipi aonyweshe ibada nyingine nje ya Qur’an na Sunnah?!.

10- Tazama: [Majallatul Manaar] (Jz. 22, Uk. 49).

"وَقَدْ كَانَ شَيْخُنَا أَبُو ثَابِتٍ مُحَمَّد بُخَيْت المُطِيْعِي... سُئِلَ عَنِ الذِّكْرِ بِهَذَا الِاسْمِ فَشَرَعَ فِي الْجَوَابِ فِيْ إِبْطَالِهِ وَإِبْطَالِ كَوْنِ آهْ اسْمًا مِنْ أَسْمَاءِ اللَّهِ تَعَالَى..."

“Na sheikh wetu Abu Thabit Muhammad Bukheit Al-Mutwii’ aliulizwa kuhusu (kusoma) dhikri kwa jina hili, akaingilia kujibu kwa kubatilisha dhikri hiyo na kubatilisha kuwa Aah آه ni miongoni mwa majina ya Allaah Ta’alaa”[11].

Kadhalika sheikh Atwiyyah Swaqri **رَحِمَهُ اللهُ** aliulizwa swali:

"مَا حُكْمُ ذِكْرِ بِعْضِ أَرْبَابِ الطُّرُقِ الصُّوْفِيَّةِ بِلَفْظِ " آهْ "؟

“Ni ipi hukumu ya dhikri ya baadhi ya viongozi wa twariqa za Kisufi kwa neno Aah”?

Akajibu:

فَإِنَّ لَفْظَ " آهْ " لَمْ يَثْبُتْ بِسَنَدٍ صَحِيْحٍ أَنَّهُ اسْمٌ **مِنْ أَسْمَائِهِ تَعَالَى..."**

“Hakika neno (Aah آهْ) halijathibiti kwa sanadi iliyo sahihi kwamba ni mojawapo ya majina ya Allaah”[12].

Halafu akakitaja kile kisa cha Mtume ﷺ na Maswahaba zake kumtembelea mgonjwa wakamkuta anatoa sauti ya kushitakia maumivu (Aah Aah), kisha alipomaliza kunukuu akasema:

"لَمْ يَرِدْ فِيْ حَدِيْثٍ صَحِيْحٍ وَلَا حَسَنٍ كَمَا قَرَّرَهُ الثِّقَاتُ"

“(Habari hiyo) haijapokewa katika hadithi Sahihi wala Hasan kama walivyothibitisha hilo wapokezi waaminifu (Thiqaat)”[13].

Takhriij ya Hadhithi hii:

Ndugu msomaji, nimetangulia kutaja kisa hiki cha kutembelewa mgonjwa akawa anaugulia maumivu kwa kusema Aah Aah, kisa ambacho kimepokewa kutoka kwa mtu mmoja anaeitwa Ismail Bin ‘Ayyaash Bin Salim Al-Ansiy Abu ‘Utba Al-Himswiy, lakini kama inavyofahamika kwamba katika Dini yetu kuna misingi madhubuti ya kuthibitisha habari kupitia wapokezi wake (wasimulizi wa habari hiyo), na hapa tutaangalia hali za watu waliosimulia habari hii, ili kufahamu kuwa je habari hii si sahihi?.

---

[11]- Tazama kibabu: [Al-Mudaawi Li’lalil Jaami’ Sswaghiir] (Jz. 3, Uk. 36-37).
[12]- Tazama kitabu: [Daarul kutubul Misriyyah] (Jz. 9, Uk. 368).
[13]- Tazama kitabu: [Daarul kutubul Misriyyah] (Jz. 9, Uk. 368).

Ndugu msomaji, ndani ya kisa hiki kuna kasoro nyingi lakini hapa tutazitaja baadhi yake tu In Shaa Allaah.

- Kasoro ya kwanza ni mpokezi: Ismail Bin Ayyaash Abu ‘Utba Al-Himswiy.

Amesema Imam Ad-Dhahabi رَحِمَهُ اللهُ katika kitabu chake Al-Miizaan akinukuu maneno ya Imam Bukhari kuhusu Ismail Bin Ayyaash, amesema:

"إِذَا حَدَّثَ عَنْ أَهْلِ بَلَدِهِ فَصَحِيْحٌ، وَإِذَا حَدَّثَ عَنْ غَيْرِهِمْ فَفِيْهِ نَظَرٌ".

“Akisimulia kutoka kwa masheikh wa mji wake ni sahihi, na akisimulia kutoka wasiokuwa hao ndani yake kunahitaji kutazamwa (kuchunguza)”[14].

Maneno hayo ya Imam Bukhari yamefafanuliwa na Imam Suyutwi رَحِمَهُ اللهُ katika kitabu chake kwa kusema:

"الْبُخَارِيُّ يُطْلِقُ: فِيهِ نَظَرٌ وَسَكَتُوا عَنْهُ فِيمَنْ تَرَكُوا حَدِيثَهُ"

“Bukhari (huwa anatumia kauli) kwa kusema: ndani yake kunahitaji kutazamwa, (au) wamemnyamazia (anazitumia kauli hizi) kwa mpokezi ambaye (wanachuoni) wameziacha hadithi zake”[15].

Kwa hiyo hadithi za Ismail ‘Ayyaash alizopokea kutoka kwa watu wa mji wa wake (Sham) ni sahihi, lakini alizopokea kutoka kwa watu wasiokuwa hao ni dhaifu, maneno kama hayo amesema pia Imam Ahmad na Ibnul Madainy رَحِمَهُمَا اللهُ :

Amesema Imam Ahmad رَحِمَهُ اللهُ :

"إِسْمَاعِيْلُ بْنُ عَيَّاشٍ مَا رَوَى عَن الشَّامِيِّيْنَ صَحِيْحٌ وَمَا رَوَى عَن أَهْلِ المَدِيْنَةِ وَأَهْلِ العِرَاقِ فَفِيْهِ ضَعْفٌ يَغْلِطُ".

“Ismail Bin ‘Ayyaash (hadithi) alizopokea kutoka kwa watu wa Sham ni sahihi, na alizopokea kutoka kwa watu wa Madina na Iraq ndani yake zina udhaifu, anakosea”[16].

Na Ismail Bin ‘Ayyaash amesimulia kisa hiki kutoka kwa wasiokuwa watu wa mji wake, kwa hiyo amechanganya na amekosea, wala haikubaliwi

---

[14]- Tazama kitabu: [Miizaanul ‘itidaal] (Jz. 1, Uk. 241).
[15]- Tazama kitabu: [Tadriibu Rraawi] (Jz. 1, Uk. 410).
[16]- Tazama kitabu: [Al-Kaamil fid Dhu’afaa] (Jz. 1, Uk. 472).

habari hii kutoka kwake, na ushahidi wa hilo ni kwamba yeye ameipokea habari hii kutoka kwa mtu mmoja anaejulikana kwa jina la Laithu Bin Abi Suleim Bin Zuneim Al-Qurashiy.

Amesema Al-Mizzi رَحِمَهُ اللهُ kuwa huyu ni mtu wa mji wa Kufa huko Iraq:

"لَيْثُ بْنُ أَبِيْ سُلَيْم بْنِ زُنَيْمٍ القُرَشِيُّ أَبُو بَكْرٍ، الكُوْفِيُّ"

“Laithu Bin Abi Sulaim Bin Zuneim Al-Qurashiy, Abu Bakri ni mtu wa Kufa”[17].

- Kasoro ya pili ni mpokezi: Laithu Bin Abi Suleim:

Amesema Ibn Hibbaan رَحِمَهُ اللهُ kuhusu Laithu Bin Suleim:

"وَلَكِن اخْتَلَطَ فِي آخِرِ عُمُرِهِ حَتَّى كَانَ لَا يَدْرِي مَا يُحَدِّثُ بِهِ فَكَانَ يَقْلِبُ الْأَسَانِيْدَ وَيَرْفَعُ الْمَرَاسِيْلَ وَيَأْتِي عَن الثِّقَاتِ بِمَا لَيْسَ مِنْ أَحَادِيْثِهِمْ كُلُّ ذَلِكَ كَانَ مِنْهُ فِي اخْتِلَاطِهِ"

“Lakini alichanganyikiwa mwishoni mwa maisha yake, mpaka akawa hakijui kile anachosimulia, akawa anageuza sanadi (wapokezi), na anazifanya Marfuu’ (hadithi) ambazo ni Mursal, na anasimulia kutoka kwa watu waaminifu kile kisichokuwemo katika hadithi zao, yote hayo yalimtokea katika wakati wa kuchanganyikiwa kwake”[18].

Kwa sababu hiyo amesema Ibn Hajar رَحِمَهُ اللهُ :

"اخْتَلَطَ جِدًّا وَلَمْ يُتَمَيَّزْ حَدِيْثُهُ فَتُرِكَ"

“Alichanganyikiwa sana (mwishoni mwa umri wake) na wala hazikuweza kupambanuka Hadithi zake, kwa sababu hiyo akaachwa”[19].

Na pia amenukuu Ibn Hajar رَحِمَهُ اللهُ kauli za Maulamaa mbalimbali wa Hadithi kuhusiana na Laithu Bin Abi Suleim, hapa nitazitaja baadhi yake:

1. Amesema Al-Haakim رَحِمَهُ اللهُ :

"مُجْمَعٌ عَلَى سُوْءِ حِفْظِهِ"

“(Maulamaa) wamekubaliana juu ya ubaya wa hifdhi yake”.

---

[17]- Tazama kitabu: [Tahdhiibul kamaal] (Jz. 24, Uk. 279-280).
[18]- Tazama kitabu: [Al-Majruuhin] (Jz. 2, Uk. 231) cha Ibn Hibbaan.
[19]- Tazama kitabu: [Taqriibu Ttahdhiib] (Uk. 464). Tarjama namba (5678).

Kwa maana anachanganya katika yale aliyohifadhi, kama tulivyoona katika maneno ya Ibn Hibbaan.

2. Amesema Al-Jauzajaani رَحِمَهُ اللهُ :

"يُضَعَّفُ حَدِيْثُهُ"

“Hadithi zake zinadhoofishwa”.

3. Amesema Ibn Ma’iin رَحِمَهُ اللهُ :

"مُنْكَرُ الحَدِيْثِ"

“Mwenye Hadithi mbaya”[20].

- Kasoro ya tatu ni mtu mpokezi anaeitwa: Buhayya:

Amesema Ibn Hajar رَحِمَهُ اللهُ :

"بُهَيَّةُ بِالتَّصْغِيْرِ لَا تُعْرَفُ"

“Buhayya kwa Tasw-hghiir (mtu huyu) hajulikani”[21].

Anakusudia jina hilo halisomwi **BAHIYYA,** isipokuwa linasomwa kwa **Tasw-ghiir (kudogoshwa) BUHAYYA.**

Kufikia hapa umejionea ndugu msomaji sifa za wapokezi wa Kisa hiki, ndani yake kuna ambao: **walichanganyikiwa, walioachwa (hadithi zao) na wasiojulikana, vipi mtu anasimama kwenye hadhira ya watu na kuzungumza kwa kinywa kipana hali ya kuwa ushahidi wake ndio huu?!**

Isitoshe amekatazwa mtu kutoa sauti ya Aah آهْ wakati wa kupiga Miayo, kwa sababu shetani huwa anamcheka mtu mwenye kufanya hivyo.

"فَإِذَا تَثَاءَبَ أَحَدُكُمْ فَلْيَضَعْ يَدَهُ عَلَى فِيهِ، وَإِذَا قَالَ: آهْ آهْ فَإِنَّ الشَّيْطَانَ يَضْحَكُ مِنْ جَوْفِهِ"

“Atakapopiga Miayo mmoja wenu basi na aweke mkono wake juu ya kinywa chake, atakaposema: Aah Aah آهْ آهْ hakika shetani anamcheka ndani kinywani mwake”[22].

---

[20]- Tazama kitabu: [Tahdhiibu Ttahdhiib] (Jz. 8, Uk. 468).
[21]- Tazama katika: [Taqriibu Ttahdhiib] (Uk. 744). Tarjama namba (8548).
[22]- Tazama kitabu: [Sunan Tirmidh] (2746).

Kwa hiyo tamko hili si jina la Allaah, wala hapana ushahidi wowote juu ya madai yao hayo, si ndani ya Qur'an, Hadithi wala kauli ya Swahaba yeyote, bali hata akili iliyosalimika haikubaliani na upuuzi huu, na mfano wa uzushi utaupata kwenye vitabu vya Mashia; kwa sababu Shia na Sufi ni bidhaa moja iliyotengenezwa kwenye kiwanda kimoja, lakini rangi tafauti, ndio maana Mashia wanaamini mafanikio yao ya kupambana na Uislamu yatatimia kwa kuwaunga mkono Masufi katika bidaa zao.

Amenukuu sheikh wa Kishia Al-Majlis kauli ya Ja'far As-Swaadiq amesema:

«آهْ اسْمٌ مِنْ أَسْمَاءِ اللهِ؛ فَمَنْ قَالَ آهْ، اسْتَغَاثَ بِاللهِ عَزَّ وَجَلَّ»

"Aah ni miongoni mwa majina ya Allaah; atakaesema Aah, ameomba ulinzi kwa Allaah Azza Wajalla"[23].

[23]- Tazama kitabu: [Bihaarul Anwaar] (Jz. 78, Uk. 202). Na kitabu: [Mustadrakul wasaail] (Jz. 2, Uk. 110). Na kitabu: [Tafsiirul Nuuri Tthaqalain] (Jz. 1, Uk. 12).

Ni kweli Nabii Ibrahim alikuwa anamdhukuru Allaah kwa kusema: Aah Aah?

Miongoni mwa shubha (hoja tata) zao wanazotumia katika kutetea uzushi wao huo ni kauli ya Allaah:

﴿إِنَّ إِبْرَٰهِيمَ لَأَوَّٰهٌ حَلِيمٌ﴾

“Hakika Ibrahim alikuwa mwingi wa kuomba (Dua) mvumilivu”[24].

Wakidai kwamba Nabii Ibrahim عَلَيْهِ الصَّلَاةُ وَالسَّلَامُ alikuwa akimdhukuru Allaah kwa neno hilo Aah: آهٍ.

Amesema sheikh wa chuo kikuu cha Azhar Muhamad Abul Fadhli رَحِمَهُ اللهُ katika fatwa yake:

"فَلَيْسَ مِن الِاسْتِدْلَالِ فِي شَيْءٍ، بَلْ هُوَ بِقَوْلِ الجَاهِلِيْنَ أَشْبَهُ؛ لِأَنَّ الآيَةَ لَيْسَ مَعْنَاهَا أَنَّهُ كَانَ يَذْكُرُ اللهَ بِلَفْظِ (أَهْ) كَمَا يَفْعَلُوْنَ بَلْ مَعْنَاهَا - كَمَا قَالَ المُفَسِّرُوْنَ - أَنَّهُ كَانَ مُشْفِقًا رَحِيْمًا"

“Hakuna hoja yoyote, bali (hoja) hiyo ni yenye kufanana zaidi na kauli ya wajinga, kwa sababu Aya hiyo haimaanishi kwamba alikuwa akimdhukuru Allaah kwa kwa kusema (Ah: أَهْ) kama wao wanavyofanya, bali maana yake kama walivyosema wanchuoni wa tafsiri: kwamba yeye (Ibrahim) alikuwa Mwenye huruma Mvumilivu”[25].

Imam Qurtubi amekusanya maneno ya Maulamaa mbalimbali kuhusu makusudio ya neno hilo (الْأَوَّاهِ) katika Aya na kuwataja wenye kauli hizo, lakini mimi hapa nitafupilizika kwa kutaja kauli peke yake:

"اخْتَلَفَ الْعُلَمَاءُ فِي الْأَوَّاهِ عَلَى خَمْسَةَ عَشَرَ قَوْلًا"

“Wanachuoni wamekhitalifiana kuhusiana na neno AWWAAHI juu ya kauli kumi na tano:

الْأَوَّلُ- أَنَّهُ الدَّعَّاءُ الَّذِي يُكْثِرُ الدُّعَاءَ.

1. “Kwamba ni Mwingi wa kuomba Dua”.

---

[24]- Surat At-Tauba/114.

[25]- Tazama: [Majallatul Manaar] (Jz. 22, Uk. 49).

الثَّانِي- أَنَّهُ الرَّحِيمُ بِعِبَادِ اللَّهِ.

2. “Mwingi wa huruma kwa waja wa Allaah”.

الثَّالِثُ- أَنَّهُ الْمُوقِنُ.

3. “Mwenye yakini”.

الرَّابِعُ- أَنَّهُ الْمُؤْمِنُ بِلُغَةِ الْحَبَشَةِ.

4. “Yeye ni Muumini, kwa lugha ya watu wa Uhabeshi”.

الْخَامِسُ- أَنَّهُ الْمُسَبِّحُ الَّذِي يَذْكُرُ اللَّهَ فِي الأرض القفر الموحشة.

5. “Mwingi wa kumsabbihi Allaah katika ardhi iliyo kame yenye ukiwa”.

السَّادِسُ- أَنَّهُ الْكَثِيرُ الذِّكْرِ لِلَّهِ.

6. “Yeye ni Mwingi wa kumdhukuru Allaah”.

السَّابِعُ- أَنَّهُ الَّذِي يُكْثِرُ تِلَاوَةَ الْقُرْآنِ.

7. “Yeye ni Mwingi wa kusoma Qur’an”.

الثَّامِنُ- أَنَّهُ الْمُتَأَوِّهُ: (**آهْ** مِنَ النَّارِ).

8. “Mwingi wa kusema Aah: (najilinda na moto)”.

التَّاسِعُ- أَنَّهُ الْفَقِيهُ.

9. “Yeye ni Faqiih (mtumbuzi wa Dini)”.

الْعَاشِرُ- أَنَّهُ الْمُتَضَرِّعُ الْخَاشِعُ.

10. “Mwenye kujipendekeza Mnyenyekevu”.

الْحَادِيَ عَشَرَ- أَنَّهُ الَّذِي إِذَا ذَكَرَ خَطَايَاهُ اسْتَغْفَرَ مِنْهَا.

11. “Alikuwa akikumbuka madhambi yake anaomba Istighfaar (msamaha)”.

الثَّانِيَ عَشَرَ- أَنَّهُ الْكَثِيرُ التَّأَوُّهِ مِنَ الذُّنُوبِ.

12. “Mwingi wa kushitakia kutokana madhambi”.

الثَّالِثَ عَشَرَ- أنه المعلم للخير.

13. “Mwalimu mwenye kufundisha kheri”.

الرَّابِعَ عَشَرَ- أَنَّهُ الشَّفِيقُ.

14. “Mpole mno”.

الْخَامِسَ عَشَرَ- أَنَّهُ الرَّاجِعُ عَنْ كُلِّ مَا يَكْرَهُ اللَّهُ تَعَالَى.

15. “Mwingi wa kutubu kuachana na kila analolichukia Allaah Ta’alaa”[26].

Na kabla yake amenukuu Imam Twabari (sheikh wa wanachuoni wa tafsiri), na mwisho wa akasema:

"وَأَوْلَى الأَقْوَالِ فِيْ ذَلِكَ عِنْدِيْ بِالصَّوَابِ، القَوْلُ الَّذِيْ قَالَهُ عَبْدُ اللهِ بْنُ مَسْعُوْدٍ، أَنَّهُ الدَّعَّاءُ"

“Na kauli iliyo bora zaidi kwangu kwa usahihi katika (maana ya neno) hilo, ni kauli aliyoisema Ibn Masoud, kwambe yeye (Ibrahim) ni Mwingi wa kuomba Dua”[27].

Kadhalika amesema Twahir Ibn ‘Ashuur **رَحِمَهُ اللهُ**:

"وَ(لَأَوَّاهُ): فُسِّرَ بِمَعَانٍ تَرْجِعُ إِلَى الشَّفَقَةِ إِمَّا عَلَى النَّفْسِ فَتُفِيْدُ الضَّرَاعَةَ إِلَى اللهِ وَالِاسْتَغْفَارَ، وَإِمَّا عَلَى النَّاسِ فَتُفِيْدُ الرَّحْمَةَ بِهِمْ وَالدُّعَاءَ لَهُمْ".

“Na naeno LA-AWWAAHU: limetafsiriwa kwa maana nyingi, zote zinarejea kwenye (maana ya) HURUMA, ima kujihurumia yeye mwenyewe (nafsi yake) kwa hiyo inafahamisha kujipendekeza (kwake) kwa Allaah na kumuomba msamaha, au kwa watu wengine kwa hiyo itakuwa maana yake ni kuwahurumia wao na kuwaombea Dua”[28].

Abu Halima Arafat,
Markaz Sheikhil Islaam Ibn Taymiyyah,
Pongwe Tanga,
18/Safar/1444H - 14/8/2022M.
Simu: 0715 263 253.

[26]- Tazama [Tafsirul Qurtubi] (Jz. 8, Uk 275-276).
[27]- Tazama [Tafsir Ttwabari] (Jz. 14, Uk. 532).
[28]- Tazama kitabu: [Tafsiri Ttan-wiir wat-Tahriir] (Jz. 6, Uk. 386).